

LBE 2009 – Migration

Episode 1:

The difficult illegal way: Senegal – Canary Islands

Author: Bettina Rühl

Editor: Thomas Mösch

Translator: Anne Thomas

Characters:

Scene 1:

Narrator (female)

Officer Guardia Civil, man, 45-50

Scene 2:

Narrator (female)

Yayi Bayam Diouf, woman, 55

Scene 3:

Narrator (female)

Cheikh Faye, man, 38

Intro:

Hujambo msikilizaji na karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga maisha Yako kuhusu uhamiaji kati ya Afrika na Ulaya. Kila mwaka maelfu ya waafrika wanaelekea ulaya kutafuta maisha bora. Baada ya miaka michache wengine wao wanarudi makwao. Lakini wengi wao wanaamua kuendelea kuishi Ulaya. Kuna watu wa Ulaya wengi pia ambao huchagua kuishi Afrika. Katika mfululizo wa makala hizi waandishi wetu wanaelezea hali tafauti walizozipitia watu ambao wamehama kutoka bara moja hadi lingine. Leo hii tunaanza na visiwa vya Canary, visiwa vilivyopo karibu na Morocco ambavyo ni sehemu ya Uhispania kwa hivyo visiwa hivyo ni sehemu pia ya umoja wa ulaya. Kila mwaka vijana wengi kutoka Afrika ya magharibi wanajaribu kuvifikia visiwa hivi kwenye safari za mashua za kutisha kupitia bahari ya Atlantiki.

Scene 1:

1. SFX: in the port of Arguineguin, Gran Canaria

2. Female narrator:

Ni saa nane usiku. Bandari ndogo ya Arguineguin, iliyo kusini mwa kisiwa cha Canary cha Gran Canaria, haina mtu.

3. SFX: Building a tent city in the port (fade under)

4. Narrator:

Muda mchache baadae wahudumu wa chama cha msalaba mwekundu wanafika mahala hapo, wanawasha jenereta na mara moja taa zenye mwanga mkali zinawaka. Na hapo wahudumu hao wanasimamisha mahema manne makubwa kwenye gati, halafu wanaleta mablanketi, vinywaji na vifurushi vya vyakula.

(fade up) **SFX: Building a tent city in the port**

5. Narrator:

Usiku wa leo "Cayuco" inatarajiwa kuwasili. Cayuco ni mashua ndogo ambazo hutumika kuwasafirisha maelfu ya watu kutoka Afrika Magharibi mfumo ambao umeibuka katika miaka ya hivi karibuni. Mwanamume mmoja kutoka "Guardia Civil", kikosi maalum cha polisi cha nchini Uhispania amekaa kwenye nguzo ya gati.

6. O-Ton Guardia Civil, eng.:

Unajua tuna maafisa wanaofanya kazi kule Afrika, maafisa wa “Guardia civil” na maafisa wa kikosi maalum cha polisi,wanaifanyia kazi FRONTEX, kwa hivyo tuna mawasiliano kati ya Afrika na Uhispania, Visiwa vya Canary. Tunabadilishana taarifa, halafu sote tunatambua mahala walipoondokea. Ni kitu cha kuvutia, lakini pia ni kazi ngumu wakati mwingine kutambua ni wapi walipoondokea .

SFX from the port continues

7. Narrator:

Mamlaka inayohusika nchini Uhispania inapoweza kutambua ni wapi mashua ilipoondokea, hapo inakuwa ni rahisi kuweza kuwarudisha wahamiaji.

8. SFX: Arrival of rescue boat

9. Narrator:

Mashua ndogo ya walinzi wa pwani ya Uhispania inaingia katika bandari ndogo ya Arguineguin. Kundi la wakimbizi wamejaa kwenye jukwaa la mashua hiyo. Walikuwa wanaelea baharini wakati walinzi wa pwani ya Uhispania walipowagundua. Mashua yao ya mbao ilikuwa imeachwa nyuma baharini.

10. SFX: Arrival of rescue boat

11. Narrator:

Wakimbizi hao wamechoka hawawezi hata kusimama. Wengi wao wanasaidiwa na maafisa wa huduma ya kwanza. Mtu mmoja anabebwa hadi nchi kavu kwa machela. Maafisa wa usalama wa Uhispania wanajitayarisha kuanza mahojiano. Na kisha wakimbizi wanapelekwa kwenye kambi ya mapokezi. Wanakingwa dhidi ya waandishi wa habari.

SFX fade down, fade up again (Change of scene!)

Scene 2:

12. SFX I of beach Thiaroye s/Mer

Atmo free and then under text:

13. Narrator:

Kilomita 1,500 kutoka katika bandari ya Arguineguin kinapatikana kijiji cha wavuvi cha Thiaroye sur Mer nchini Senegal. Wakati huu huenda ikawa hakuna mtu aliyesafiri kwenye mashua hii kutoka huko, lakini vijana wengi kutoka eneo hilo wameingia Ulaya kupitia visiwa hivyo vya Canary siku zilizopita. Vile vile pia wengi wao wamebakia baharini – Kwa sababu hawakuonekana na mashua za waokoaji.

15. O-Ton Yayi Bayam Diouf, French :

"Sisi wote ni wanawake tuliokumbwa na mashaka haya ya uhamiaji, tumewapoteza watoto wetu au hata waume zetu. Walisafiri na mashua za uvuvi kwenda Ulaya."

SFX Beach cross fade with:

14. SFX: in the association's building

Free for a short while and then under the text

15. Narrator:

Yayi Bayam Diouf ni mwanzilishi wa kikundi cha wanawake cha Thiaroye. Katika kijiji hiki kilichopo nje ya mji mkuu wa Dakar, nchini Senegal, kutoka jadi watu wa huko waliishi kutokana na mapato ya baharini. Lakini sasa maisha yanazidi kuwa magumu . Zamani sehemu hiyo ilikuwa na utajiri mkubwa, lakini kutokana na shughuli za uvuvi kukithiri , bahari ya Senegal haina tena samaki wa kutosha siku hizi. Mtoto wa kiume wa Yayi Bayam Diouf alikuwa mvuvi pia – alijifunza kazi hiyo kutoka kwa baba yake.

16. O-Ton Yayi Bayam Diouf, French :

"Aliporudi kutoka kuvua aliweka fedha zake. Alikuwa na akaunti. Sikujua kuwa alikuwa anakusanya fedha zake. Alipoondoka aliniambia kuwa wanakwenda safari ya kuvua huko Nouadhibou kwa sababu hapa hakuna samaki tena ."

17. Narrator:

Kwa mwezi mzima kijana huyo wa miaka, 26 na rafiki zake walijaribu kuingia katika nchi jirani. Halafu Yayi Bayam Diouf alipata simu. Ilikuwa mwanzoni mwa mwezi wa Aprili mwaka wa 2006.

18. O-Ton Yayi Bayam Diouf , French :

"Aliniambia kuwa hawajapata chochote na kwa hivyo walikuwa wanaenda Uhispania kupitia visiwa vya Canary. Alinieleza kuwa kule kuna kazi nyingi na kwamba atanitumia fedha za matumizi ya nyumbani."

19. Narrator:

Picha ya mtoto wa Yayi Bayam Diouf iko nyuma ya meza yake. Bila shaka ilipigwa na mtaalamu kwani ilitoka vizuri sana. Kijana huyo ni mrefu na anaonyesha kuwa ni kijana mwenye nguvu. Anaonyesha kuwa ni mtu anaejiamini na tayari kupambana na maisha. Usiku wa mwisho kabla hajaondoka alimwita mama yake na kumueleza kuwa anataka kwenda katika visiwa vya Canary pamoja na vijana wengine 80 kutoka Thiaroye. Alisema kuwa yeye ni mtu wa 81 na pia ndie kapteni wa mashua hiyo.

20. O-Ton Yayi Bayam Diouf , French :

"Walisafiri kwa mashua mbili ili wapate kuchangamshana na pia kupunguza uchofu. Kutokana na yale niliyoambiwa, ni kwamba pale walipofika bahari kuu, vijana kutoka kwenye mashua ya pili waliona kuwa mashua aliyokuwemo mwanangu ilikuwa inaanza kujaa maji. Walimwambia asimamishe mashua yake au apunguze mwendo na kwamba walikuwa wameanza kuviona visiwa vya Canary. Waliwaaambia kuwa wataharakisha halafu watume watu waje wawaokoe. Basi waliondoka na huku nyuma mvua kubwa ikanyesha na kusababisha mawimbi makubwa yaliyopita mita 13. Pengine hiyo ndio ilikuwa sababu ya kuvunjika kwa mashua yao, na wote walizama baharini. Wakati wenzao waliporudi saa moja au mbili baadae, waliona chupa, viatu, peremende vikienea baharini – waliwajulisha walinzi wa pwani ya Uhispania lakini hawakumpata mtu hata mmoja walipofika. Wala miili haikupatikana pia. Ndugu zangu walinipigia simu na wakanieleza kuwa mashua aliyosafiria mwanangu ilizama na wote waliokuwemo ndani walikufa."

22. Narrator:

Mtoto wa Yaya Bayam Diouf alikuwa kapteni ndio maana alikuwa wa kwanza kupewa taarifa. Na yeye aliwajibika kutoa habari hizo mbaya kwa wazazi wengine hapo kijijini. Ilimbidi kuwaeleza ndugu wahusika kutoka familia 80 tofauti.

23. O-Ton Yaya Bayam Diouf, French :

"Ulikuwa ni wakati mgumu sana, mgumu sana. Waliuliza maswali: 'Wako wapi watoto wetu? Mtoto wako ndie aliyekuwa anaendesha mashua iliyowabeba watoto wetu.'"

Scene 3:

24. SFX: of beach in Thiaroye: Sheep, Waves, Children, Muezzin

Free for a short time, then under text until the next voice clip

25. Narrator:

Baada ya mkasa huo, Yaya Bayam Diouf alianzisha kikundi hicho cha wanawake cha "Kupambana na Uhamiaji Haramu kutoka Senegal". Mara nyingi kina mama ndio hugharamia safari za watoto wao. Mashua nne huondoka kila siku nje ya mji mkuu wa Dakar zikiwa na watu 80 au zaidi ndani ya kila mashua. Cheikh Faye ana miaka 38 na amejaribu safari za aina hiyo mara sita kutaka kuingia Ulaya.

26. O-Ton Cheikh Faye, French :

"Kilichonishawishi ni hawa vijana kutoka kwenye kijiji chetu ambao waliondoka kwenda Uhispania kwa ndege. Vijana hawa wangerudi hapa na kununua magari mazuri, na kujenga nyumba nzuri– walikuwa wakituambia: 'Msikae hapa Senegal, njooni Ulaya, mtaweza kuwapeleka

wazazi wenu Mecca, mtajenga nyumba nzuri, mtapata wake wazuri na magari mazuri.' Kama hufikirii vyema, ukisikia hizi habari basi unadhani kuwa utaweza kwenda Ulaya ukatengeneze mamilioni."

27. Narrator:

Alipokuwa na miaka 29, Cheikh Faye alijaribu kwa mara ya kwanza kutaka kwenda Ulaya. Ilikuwa ni mwaka 2000. Alijaribu kwenda Gibraltar kutokea Tangiers lakini injini ya mashua ilikata katikati ya maji marefu, ni bahati kubwa alinusurika. Baada ya hapo alikuwa kati ya Mauritania, Morocco na Senegal – kwa bidii akijaribu kutafuta njia ya kumfikisha Ulaya. Siku moja alipokuwa nyumbani huko Thiaroye, rafiki yake alimpigia simu.

28. O-Ton Cheikh Faye, French :

"Aliniambia 'Cheikh, usikae Senegal, njia imepatikana. Ukienda Mauritania na laki moja na nusu Utafika Uhispania ndani ya siku mbili.' Nikazungumza na rafiki zangu halafu tukaondoka kwa mashua. Tulikuwa 80 na tulilipa kila mmoja CFA laki tatu na nusu. Tulikwenda hadi Saint Louis na tukafika Uhispania."

29. Narrator:

Lakini alipofika tu, Cheikh Faye alikamatwa na kurudishwa kwao. Alijaribu tena baada ya muda mfupi.

30. SFX: Outboard engine starting up

Free, and then fade out under voice clip

31. O-Ton Cheikh Faye, French:

"Kulikuwa na mawimbi mengi katika bahari ya Atlantiki. Mawimbi yalikuwa na nguvu mno yalituangusha. Tulikuwa watu wengi, na tulianza kupata

shida siku ya pili yake. Iliendelea kwa siku nane tulizokuwa baharini. Vijana walikuwa wagonjwa na walikuwa wanatapika , mwishowe watu wakaanza kufa. Tulikaa na maiti hizo kwa siku mbili au tatu halafu na sisi pia tukaanza kuwa na matatizo, basi tukazitupa maiti hizo majini. Tultitupa maiti tano wakati wa safari yangu ya kwanza."

32. **Narrator:**

Cheikh Faye na wenzake waliokolewa na meli ya mizigo. Kwa kuwa alikipiga chenga kifo, Cheikh Faye hakukata tamaa. Alijaribu mara nyingine mbili lakini hakufanikiwa. Mara ya pili yeye ndie aliyekuwa kapteni.

33. **O-Ton Cheikh Faye, French :**

"Tulipoingia kwenye maji makubwa tu injini ilikata moto. Injini ya spea pia haikufanya kazi na wimbi kubwa lilipokuja mashau yetu ilivunjika. Maji yalijaa ndani. Mdogo wangu alikufa mbele ya macho yangu. Alikuwa na duka na mradi wa kushona hapa Thairoye."

34. **Narrator:**

Kwa mara nyingine tena waliokolewa na meli ya mizigo. Cheikh Faye aliporudi Thiaroye, Yayi Bayam Diouf alimpigia simu . Alimsihi akubali kufanya kazi na yeye, kazi ya kuwahamasisha vijana kuhusu hatari za kujaribu kuhamia katika nchi za kigeni kinyume cha sheria. Na wakati huu, Cheikh Faye aliamua kujiunga na mradi huo.

35. **O-Ton Cheikh Faye, French :**

"Rafiki zangu karibu 50 wamenitoka, watu ambao nilikuwa nao maishani.katika miaka ya 2000, 2005 na 2006 tulicheza mpira pamoja – mvua ilipokuwa inanyesha hatukuweza kwenda baharini kwa hiyo

tulicheza mpira, tulikuwa na timu yetu lakini sasa karibu wote wamefariki. Kufikia mwaka 2007, hatukuwa na timu tena.”

36. Narrator:

Yayi Bayam Diouf alianza kuweka hesabu ya waliofariki kutoka kwenye kijiji chake. Baada ya mwaka mmoja aliwasilisha hesabu hiyo – ilikuwa ni vijana 241 walioangamia kwa kuzama na vijana 156 hawajulikani walipo.

37. SFX: SFX I of beach Thiaroye s/Mer (*Atmo from the sea in Thiaroye*)

Fade out

Outro:

Na huo ndio mwisho wa makala haya ya leo katika Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu uhamiaji. Mwandishi wetu leo hii ni Bettina Rühl. Asante msikilizaji kwa kuwa nasi. Iwapo ungetaka kujifahamisha zaidi kuhusu swala hili au kama unataka kukisikiliza tena kipindi cha leo au vipindi vinginer vya Noa Bongo Jenga Maisha Yako, tafadhali tembelea tovuti yetu. Anuani yetu ni: www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati ujao. Kwaheri.